


# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

### TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA IRINGA



Kumb. Na. IDC/S.20.III/66



06 JUNI, 2022

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa anakaribisha maombi ya kazi kwa Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za **Dereva Daraja la II** na Katibu **Mahsusi Daraja la III**. Tangazo hili ni kutokana na Kibali cha Ajira chenye **Kumb. Na.FA.97/228/01/09**. cha tarehe 13 Mei 2022, Kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nafasi hizo za kazi ni hizi zifuatazo:

### 1.0. DEREVA DARAJA LA II. (NAFASI (4)

#### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI:

- Awe amehitimu Kidato cha Nne (Form IV). Awe na leseni Daraja **E** au **C** ya uendeshaji Magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhulia mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza

#### 1.2 MAJUKUMU YAKE:

- kuendesha Magari ya Halmashauri.
- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari ya kikazi
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- Kutunza na kuandika daftari ya safari (Log Book) kwa safari zote
- Kufanya usafi wa gari
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake

**NGAZI YA MSHAHARA TGS B**

MKURUGENZI MTENDAJI [W]  
HALMASHAURI YA WILAYA  
IRINGA



## **NGAZI YA MSHAHARA TGS B**

### **2. KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III (NAFASI (3)**

#### **1.2 SIFA ZA MWOMBAJI:**


- Awe amehitimu Elimu ya kidato cha Nne na amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya 3.
- Awe amefaulu somo la hati mkato ya Kiswahili na kiingereza maneno 80 kwa dakika na awe amepata mafunzo ya kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali awe
- Cheti katika program za:-  
**Windows, Microsoft Office, Internet, email na Publisher.**

#### **1.2 MAJUKUMU YAKE:**

- Kuchapa barua, taarifa na Nyaraka za kawaida.
- Kusaidia kupokea wageni, kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, Miadi, Wageni, tarehe za Vikao, Safari za Mkuu wake na Ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anamofanyia kazi, na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- Kusaidia kutafuta na kusaidia kumpatia Mkuu wake majalada, Nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo Ofisini.
- Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa na kuyapeleka sehemu walipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu inayohusika.

#### **MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WA KAZI ZOTE.**

- i. Mwombaji awe ni Raia wa Tanzania
- ii. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- iii. Maombi yote yaambatishwe na nakala ya cheti cha Taaluma, cheti cha Kidato cha Nne, cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha uraia au namba ya NIDA.
- iv. Maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) ikiwa na anuani, namba za simu za kuaminika, majina matatu ya wadhamini na picha mbili (Passport Size) za hivi karibuni.
- v. Vyeti vyote vya Taaluma, Kidato cha Nne na cheti cha kuzaliwa vithibitishwe na Hakimu/Wakili anayetambulika na Serikali.
- vi. Aidha, uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria na Mamlaka zinazohusika.
- vii. Watumishi waliopunguzwa kazi/kufukuzwa kazi Serikalini hawaruhusiwi kuomba.



- viii. Mwombaji yeyote ambaye hatazingatia mojawapo ya masharti au vigezo tajwa hapo juu maombi yake hayatashughulikiwa.
- ix. Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa na iliyoandikwa kwa Kiswahili au Kiingereza na barua hiyo ielekezwe kwa:-



**Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Iringa,  
S.L.P. 108,  
IRINGA.**

Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe **20 Juni, 2022** saa **09:30 Alasiri.**

**Imetolewa leo tarehe**

**07 JUNI, 2022**

na



**Bashir P. Muhoja  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
IRINGA.**

Nakala: Mbao za Matangazo

: Tovuti ya Halmashauri

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA  
IRINGA**

